**Ripoti ya mafunzo ya kuendesha baiskeli kwa usalama na kwa kufata sheria barabarani**

**Shule ya Msongola**
**18 – 21 Novemba 2008**

**Walimu walio shiriki**
Filbert Mbecha
Hamad Bwaja
Edgar Paulo
Hussein Hamza
Bashiri Rashidi
Frank Peter

## Ripoti

Mafunzo yalifanyikiwa kwa siku nne. Wanafunzi wa sekondari 60 walifundishwa siku zote nne. Walikuwa na umri kati ya miaka 14 mpaka miaka 18, na wote walikuwa form 1. 49 walikuwa wavulana na 11 wasichana. Wanafunzi 55 wa shule ya msingi walifundishwa siku mbili za mwisho. Walikuwa na umri kati ya miaka 10 mpaka miaka 18 na walikuwa standard 2, 3, 4, 5 na 6. 39 walikuwa wavulana na 16 walikuwa wasichana. Tuliwagawa wanafuni wa shule ya sekondari katika madarasa mawili mkondo A na B.

Mokondo A walifundisha walimu wafuatao: Filbert Mbecha, Hussein Hamza, Bashiri Rashidi. Mkondo B walifundisha walimu wafuatao: Hamad Bwaja, Edgar Paulo, Frank Peter.

Tulianza kama ifuatavyo:

1. Five E's

Ili kupata uhakika kama wanafunzi wameelewa juu ya somo hili tuliwapa nafasi ya kujadiliana katika makundi kuhusu malengo ya mitano ijayo, na tumekusanya maoni yao.

2. Sehemu za baiskeli

Baada ya kuwafundisha na kuzitambua sehemu za baiskeli na kazi zake, tuliwapa nafasi wanafunzi kuonyesha sehemu za baiskeli na kazi zake. Tulichora baiskeli na kuonyesha sehemu zake na kazi zake, halafu tukafuta na kila mwanafunzi alipata nafasi ya kuonyesha na kuandika sehemu zake ubaoni.

3. Uvaaji wa Helmet na Jacket reflector na umuhimu wake

Baada ya kuwafundisha, tulitoa nafasi ya kufanya majadiliano katika vikundi fadia za kuvaa helmet na reflector jacket na hasara na tulikusanya maelezo yao.

4. Kuchecki baisikeli yako kabla ya kuondoka

Tuliwafundisha darasani na tulitoka nje ya darasa na kuwapa nafasi ya wanafunzi kutoa maelezo ya matatizo waliyoyaona kwenye baiskeli zao.

5. Vipi kupanda baiskeli

Tulielekeza wanafunzi darasani na tulitoka nje ya darasa kufanya kwa vitendo.

6. Kudhibiti baiskeli yako na zoezi la kulenga jagi hadi jagi, kushika brake kwa haraka na mashindano ya pole pole

Tuliwafundisha wanafunzi darasani na kwa vitendo nje ya darasa, na tulichukua majina ya wanafunzi waliofanya vizuri kwa kila zoezi.

7. Kupinda kushoto na kulia

Tuliwaelekeza wanafunzi darasani na kwa vitendo nje kuonyesha alama za mikono na ishara.

8. Kuzitambua alama za barabara, wapi uendeshe baiskeli, makutano ya barabara

Tuliwafundisha darasani tu kw akuwaelekeza alama ambazo muhimu kwa mpanda baiskeli na baadhi ya zingine kama ziada kwa kubandinga bango la michoro ya alama za barabarani ubaoni ambazo tulipewa na Allan Jones wa Wizara wa Miundumbinu wakati tulipoalikwa kwenda kutoa mafunzo kwa wanafunzi siku ya nenda kwa usalama Morogoro.

9. Makutano yanayoongozwa na taa au traffic police

Tuliwafundisha kama kuna traffic police wafuate maelekezo ya traffic police na kama ni mataa basi wafuate mataa.

10. Barabara ya kweli

Walimu tulitoa mafunzo hayo darasani na kwa vitendo katika barabara kubwa na wanafunzi kutoka msongola hadi makutano ya barabara inayotoka Mbalaga na m’mbande kwa kuwagawa makundi na kila kundi liliongonzwa na mwalimu. Jumla ya makundi yote yalikuwa sita makundi matano wanafunzi wa secondary and moja wa shule ya msingi msongola. Makundi yaliongozwa kama ifuatavyo:

Kundi la kwanza ni wa shule ya msingi lililoongozwa na Hussein Hamza, Edgar Paulo, Frank Peter, Bashiri Rashidi, Hamad Bwaja, Filbert Mbecha. Tukishirikiana na mwamlimu Hatibu Hamisi ambaye ni wa shule ya msingi tuliyeshirikianaye katika mafunzo chuo cha Taifa cha usafirishaji NIT.

Mwisho mkuu wa shule anatoa salam kwa viongozi wa UWABA hasa katibu ambaye anawasiliana naye kwa simu tu. Angependa siku moja kuonana na kufahamiana kwa sura.

Wanafunzi walijaza fomu ya “evaluation”. Tuligawa cheti, helmet 60 na jaketi za reflecta 48 kwa wanafunzi.

Taarifa hii imeandaliwa na walimu wote walioshiriki kutoa mafunzo msongola school na kuandikiwa na mkuu wa msafara Filbert Mbecha.

Changamoto/Challenges tuliyopata walimu tulioshiriki utoaji wa mafunzo na mitazamo yetu ili kufanikisha mpango wa utoaji wa mafunzo haya kwa siku zijazo:

1. Yaangaliwe maslahi kwa walimu wanaopata nafasi ya kwenda kufundisha ili kufundisha kwa moyo zaidi.
2. Vifaa vya kufundisha viboreshwe kama vile:
   - chalk, pen na karatasi
   - mwongozo uboreshwe katika mfumo wa kitabu
   - majagi kwa ajili ya mashindano ya pole pole
   - walimu wapelekwe English course ili kukabailiana na upeo wa wanafunzi tunao kwenda kuwafundisha kufahamu lugha ya kiingereza
   - walimu wawe na baiskeli zenye sifa

3. Walimu wa shule husika tunayo kwenda kufundisha tuwahusishe katika posho isiyo zidi walimu wawili ili kuleta ukaliba na kuwapa moto wa kuwahamasisha wanafunzi kushiriki mafunzo kwa wingi
4. Pawepo na kamera ya chama ambayo itasaidia kuchukua matukio katika mafunzo ya vitendo wakati tunapokuwa mafunzoni
5. Ni muhimu kufanya maboresho katika vyeti tunavyotoa kwa waliotimu wa mafunzo ya usalama kwa wapanda baisikeli ili kuvijengea heshima na usamani, kwa sababu hakuna shirika lolote lisilo la kiserikali ambalo hutoa vyeti hivyo kwa Dar es Salaam au Tanzania ni UWABA peke yake
6. Siku ya kuhitimu mafunzo utoaji wa vyeti aalikwe mkuu wa kikosi cha usalama barabarani kanda ya Dar es Salaam au mwenyekiti wa baraza la usalma la taifa mheshimiwa Abasi Kandoro ambaye ni mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam kama mgeni rasmi
7. Muhimu kuweka nembo ya UWABA kama kwenye fulana katika reflector jaket tunazogawa mashuleni ili kuitangaza UWABA
8. Muhimu kushirikisha vyombo vya habari media kama vile redio, magazeti, TV, mfano TBC, ITV, Channel Ten. Siku ya kuhitimu mafunzo ya vitendo barabara kubwa na zoezi zima la utoaji wa vyeti na hotuba ya mgeni rasmi ili kutangaza UWABA kwa kasi zaidi Dar es Salaam na nchi nzima
9. Kuhakikisha video yetu ya vitendo vya kuendesha baiskeli kwa usalama tunaionyesha na kuitolea maelezo katika chombo cha habari kama redio au TV ili kuhamasisha kuelimisha ili kutekeleza malengo yetu ya miaka mitano

Ni mitazamo ya walimu walioshiriki utoaji wa mafunzo msongora school na kuandikwa na mkuu wa msafara Filbert Mbecha.

Maoni yetu

- Pawepo projector ya chama kwa ajili ya mafunzo wakati tunapokuwa tunafundisha

- Pawepo na pesa ya ziada zarura kwa ajili ya kukabiliana na matukio ambayo huwa tokea walimu wanapo kuwa mafunzoni
- Kwa kila mwalimu alipwe Tsh 15,000 kwa siku
- Walimu wasiozidi wawili ambao tuma shirikaina nao tokea mwanzo wa mafunzo mpaka mwisho, kwa kila sshule tutakayo kwenda wapate posho ya Tsh 5,000 kila mwalimu.
- Pesa kwa ajili ya zarula emergency fund yaangaliwe mazingira ya shule ya walimu wanyokwenda kufundisha
- Gharama ya guest kwa kila mwalimu kwa siku iwe Tsh 5,000